CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA (THTU)

RIPOTI YA KAMATI YA UCHAMBUZI NA USHAURI KUHUSU BAJETI KUU YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

YALIYOMO

YALIYOMO ii

SHUKRANI iii

MUHTASARI iv

VIFUPISHO VYA MANENO vi

DIBAJI vii

1 UTANGULIZI 1

2 MIONGOZO MIKUU YA MAANDALIZI YA BAJETI 1

2.1 Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 1

2.2 Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015–2020 2

2.3 Mpango wa Maendeleo wa Taifa 3

3 MWENENDO WA BAJETI YA TAIFA 4

3.1 Mchakato na Vipaumbele vya Bajeti 4

3.2 Sera, Mwenendo na Tathmini ya Bajeti 5

3.3 Vipaumbele Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20 7

3.3.1 Kilimo, Ufugaji na Uvuvi 8

3.3.2 Viwanda, Biashara na Uwekezaji 8

3.3.3 Miradi ya Miundombinu 8

4 MAPENDEKEZO YA UBORESHAJI WA BAJETI YA TAIFA 9

4.1 Utekelezaji wa Sera ya Viwanda 9

4.2 Uimarishaji wa Mapato Kuongeza Uwezo wa Serikali 10

4.3 Maboresho ya Mifumo ya Kukusanya Kodi 13

4.4 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maslahi ya Wafanyakazi 17

4.5 Ushirikishwaji wa vyama vya Wafanyakazi katika mikakati mbalimbali 21

5 HITIMISHO 23

6 REJEA 23

SHUKRANI

Uchambuzi huu wa maandalizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20 umeandaliwa ili kuisaidia serikali, bunge na wadau wengine wa maendeleo katika kuandaa bajeti yenye tija itakayosaidia katika kufikia malengo ya uchumi wa kati unaotegemea viwanda uliofungamanishwa na kuboresha maisha ya watanzania wakiwemo wafanyakazi.

Kwa niaba ya Uongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), shukrani za dhati ziende kwa kamati ya uchambuzi wa bajeti iliyohusisha wataalamu wanachama kutoka taasisi za elimu ya juu wakishirikiana na uongozi wa THTU Taifa katika mchakato wa kuchambua bajeti na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha bajeti ya nchi: Dkt. Paul Loisulie (THTU Makao Makuu), CPA Aisha Kapande (THTU Makao Makuu), Dkt. Alex Reuben Kira (UDOM), Dkt. Lutengano Mwinuka (UDOM), Ndg. Ngussa Kinamhala (CBE), Ndg. Deo Shao (UDOM), CPA David Mwakapala (UDOM), Ndg. Bonaventure Mshibika (IAA) na Ndg. Salum Hamisi (THTU Makao Makuu). Uchambuzi wa maandalizi haya ya bajeti umezingatia miongozo, sera, mipango na mikakati ya nchi na malengo mahususi ya THTU.

Zaidi ya hayo, uongozi wa THTU kwa ujumla unatambua mchango wa wanachama wake wote katika kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa ili kufikia malengo yanayotarajiwa kwa wakati.

© Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), 2019
Sehemu yoyote ya Ripoti hii inaweza kunakiliwa kwa matumizi yasiyo ya kibiashara, kwa sharti kwamba chanzo kitatambuliwa na nakala mojamoja ya chapisho itatumwa kwa THTU.

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU)
S.L.P 35928 DAR ES SALAAM, Tanzania
Simu: 022 2401581, Nukushi: 022 2401582
Wavuti: www.thtu.or.tz, Barua pepe: thtuhq@gmail.com

MUHTASARI

Wafanyakazi ni wadau muhimu katika kujenga uchumi wa taifa. Kuna uhusiano wa karibu kati ya wafanyakazi na sekta nyingine zote katika uchumi. Kipato anachopata mfanyakazi aliyeajiriwa au kujiajiri kwa namna moja au nyingine kinagusa na kufika katika maeneo tofauti kwa njia ya wao kukidhi mahitaji mbalimbali ya bidhaa na huduma.

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongoza harakati za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zitakazoiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Katika kuchambua bajeti kuu ya serikali, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inaangazia malengo ambayo ni kuhakikisha kuwepo kwa jamii iliyoeleimika vema na inayojifunza na kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine. Sambamba na hili, Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21) vinatoa vipaumbele katika kufikia malengo husika. Vipaumbele hivyo ni pamoja na ustawi wa wananchi; kuondoa umaskini na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana; ukuaji wa uchumi (kufikia asilimia 10); mfumuko wa bei (wastani usiozidi asilimia 5); na urari wa biashara na ukuaji wa sekta ya kilimo.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 serikali imefanya juhudi katika kutafuta mbinu mbadala za kuongeza na kuimarisha mazingira ya kukusanya pato la ndani. Juhudi hizi zilijumuisha kufanya marejeo ya baadhi ya sheria za kodi ili ziweze kuendana na mazingira ya nchi yaliyopo. Malengo makuu ya kisera katika kuongeza makusanyo ya mapato ni pamoja na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija, kuongeza utumiaji wa mifumo ya kielektroniki katika ukusaji wa mapato, kuendelea kuboresha usimamizi na ukaguzi kwenye mipaka ya nchi, bandari na viwanja vya ndege, na kupanua wigo wa mapato.

Hata hivyo, ufanisi wa makusanyo upande wa Serikali za Mitaa umekua duni katika kipindi kirefu sasa. Kwa mfano, kwa wastani wa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni asilimia 79 tu ya makusanyo yalipatikana ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, serikali imeainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyotazamiwa kugharimia shughuli za maendeleo. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa mapato ya utekelezaji wa bajeti unatia shaka katika kufikia lengo lililokusudiwa. Mathalani Katika kipindi cha mwaka

2016/2017 kati ya TZS trilioni 11.8 zilizotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo ni kiasi cha TZS trilioni 6.4 tu sawa na asilimia 55 ndicho kilipatikana katika kutekeleza lengo. Vivyo hivyo, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ambapo kati ya TZS trilioni 11.4 ni TZS trilioni 6.5 pekee sawa na asilimia 57 zilitolewa. Hali hii ya kushindwa kutekelezeka kwa malengo ya mpango wa maendeleo inatokana na ukusanyaji hafifu wa mapato ya ndani na utegemezi wa fedha za mikopo na fedha za wafadhili kutoka kwa wahisani.

Ufanisi wa utekelezaji wa sera ya viwanda utasaidia sana kuongeza mapato ya serikali na hivyo kuiwezesha kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Ili kufikia ufanisi huo, THTU inapendekeza namna bora zaidi ya kutekeleza sera ya viwanda ikiwa ni pamoja na Uimarishaji wa Makusanyo Mapato ya ndani ikihusishakuongeza Uwezo wa Serikali kuibua na kubuni vyanzo vipya; Maboresho ya Mifumo ya Kukusanya Kodi hasa kuimarisha matumizi ya TEHAMA; Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maslahi ya Wafanyakazi; mabadiliko katika Sheria za Kodi na muhimu zaidi Ushirikishwaji wa vyama vya Wafanyakazi katika mikakati mbalimbali ya serikali.

VIFUPISHO VYA MANENO

ASDP II	**Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili**
CBE	**Chuo cha Elimu ya Biashara**
CCM	**Chama Cha Mapinduzi**
FYDP	**Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano**
GePG	**Mfumo wa Malipo Serikalini**
GOT-HOMIS	**Mfumo wa Kielektroniki wa Kuendesha Hospitali**
IAA	**Chuo cha Uhasibu Arusha**
ILO	**Shirika la Kazi Duniani**
ITU	**Shirikisho la Mawasiliano la Kimataifa**
LESCO	**Baraza la Kazi la Jamii na Uchumi**
MKUKUTA	**Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini**
TEHAMA	**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**
THTU	**Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania**
TRA	**Mamlaka ya Mapato Tanzania**
UDOM	**Chuo Kikuu cha Dodoma**
VAT	**Kodi ya Ongezeko la Thamani**

DIBAJI

Kuhusu Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU)

Chama cha wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu Tanzania (THTU) kimeanzishwa kisheria kutetea uboreshaji wa maslahi mbalimbali ya wafanyakazi katika taasisi hizo. Utetezi huu unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu, miongozo na nyaraka mbalimbali za serikali au taasisi husika. Kauli mbiu ya THTU ni hii; **Nia na Mwelekeo ni Kujenga Daima, Taifa Kwanza.**

Kihistoria, uanzishwaji wa vyama vya wafanyakazi umejikita katika harakati zaidi na hivyo kujenga sura ya kutoaminiana kati ya mwajiri na wafanyakazikatika utekelezaji wa maslahi ya wafanyakazi. Mabadiliko ya kisheria, kimfumo na kimuundo yamekuwa yakitokea katika uendeshaji wa vyama hivi na kupelekea kupungua kwa utamaduni wa kutoaminiana uliokuwepo awali.

Kutokana na mabadiliko hayo tajwa, uanzishaji wa THTU umejielekeza katika kuboresha mbinu za kutetea maslahi ya wafanyakazi. Kauli mbiu ya THTU ya **Nia na mwelekeo ni kujenga daima, Taifa kwanza** imebuniwa kwa lengo la kutoa muelekeo mpya na mbinu za kisayansi katika kutetea maslahi ya wafanyakazi. Mbinu za kisayansi ni kufanya utafiti na kuonesha kitakwimu na kiuhalisia katika kujenga hoja pamoja na kuishauri serikali namna bora ya kuimarisha uchumi na hatimae kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Sheria za Tanzania zimeweka utaratibu mzuri wa kuongoza uendeshaji wa vyama vya wafanyakazi na namna ya kuwasiliana na mwajiri. Mfano wa taratibu hizo zilizowekwa kisheria ni pamoja na majadiliano kazini, uanzishwaji wa mabaraza ya wafanyakazi na uwakilishi wa wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi kwa kutaja machache. Kutokana na kauli mbiu ya THTU, tunaona tuna deni kubwa katika taifa hili kutoa mchango wetu kwa ustawi wake na kupata maendeleo endelevu na hatimae sisi wafanyakazi kunufaika moja kwa moja.

Ni kwa msingi huo ulioelezwa hapo juu, THTU inaona ina wajibu wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa hili katika kufikia malengo yanayotarajiwa kwa wakati. Kauli mbiu hii **inatuhamasisha sisi THTU kuwa washirika wa maendeleo na si watazamaji.** Hii maana yake ni kwamba tukishiriki kikamilifu katika kukuza pato la taifa, nasisi wafanyakazi tunafaidika moja kwa moja maana ni washirika. Katika dhana ya ushirika katika maendeleo, kila upande una kitu cha kuchangia kwa manufaa ya pamoja.

Jambo moja muhimu la kuweka bayana ni kwamba THTU ina hazina kubwa ya wanachama wenye viwango na weledi mkubwa wa elimu waliotabaharia/bobea katika nyanja mbalimbali. Ili kufikia azma ya kutetea uboreshwaji wa maslahi ya wafanyakazi, THTU imeunda kikosi kazi cha kufanya uchambuzi wa namna bora ya kutambua maslahi ya wafanyakazi kupitia bajeti kuu ya serikali ya mwaka 2019/2020. Uchambuzi umejikita zaidi katika masuala yote yahusuyo uandaaji wa bajeti yakiwemo sera, sheria kanuni na miongozo mbalimbali, vyanzo vya mapato, uwiano wa mapato na matumizi kisekta na mengine. Lengo kuu la uchambuzi huu ni kupendekeza njia nzuri ya kumnufaisha mfanyakazi bila kuathiri mwenendo mzima wa uendeshaji wa nchi

Tumejaribu kutafakari kidogo mambo makuu manne ambayo Baba wa Taifa letu tukufu alibainisha kuhusu maendeleo ya taifa lolote. Katika mambo hayo manne, tunapaswa kujiuliza tumepatia wapi, tumekosea wapi au tunakosa nini zaidi na ni nini cha kuongeza. THTU imetafakari na kuongeza jambo moja ambalo tunadhani linafaa katika kuongoza harakati za kufikia Tanzania ya viwanda na hatimae uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi. Mambo hayo kwa muhutasari ni;

a) Ardhi - tuna ardhi ya kutosha yenye kila aina ya rasilimali kuliko nchi nyingi za Afrika. Urasimishaji na mipango bora ya ardhi ni muhimu katika ukuaji wa sekta mbalimbali kama vile kilimo, uvuvi na ufugaji ambazo mazao yatokanayo na sekta hizo yanachangia ukuaji wa viwanda katika kufikia lengo la nchi la uchumi wa kati kufikia 2025.
b) Watu - watanzania tuko zaidi ya milioni hamsini kwa sasa. Hii inamaana kwamba watu wapo. Labda tujadili mambo yahusuyo; maarifa, ujuzi, uzalendo, uadilifu, mtazamo, weledi, uchapakazi na mengine kama yanatusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo kiufanisi.
c) Uongozi bora –kwa maana ya dhamira, uwezo na mikakati ya viongozi wa ngazi zote kuonesha njia na maono sahihi kuwaelekeza watu kufikia uchumi wa kati lakini kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.
d) Siasa safi –kwa maana ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayoratibu uendeshaji na mwenendo mzimawa siasa ambayo huleta tija na ustawi wa kiuchumi na kijamii
e) **Wanasiasa – inafahamika kwamba wanasiasa wana ushawishi mkubwa katika nchi. Matendo yao, matamshi yao na mienendo yao kwa ujumla yana athari kubwa katika kufikia malengo tarajiwa kiuchumi na umoja wa kitaifa.**

Kwa kuzingatia mambo hayo manne, tunajifunza kitu kimoja kikubwa ambacho ni umuhimu wa kila mmoja kuchangia maendeleo ya nchi katika nafasi yake. Ardhi ndiyo

kitu pekee ambacho kinategemea yale mengine matatu. Hivyo basi, THTU imejikita katika kutoa mchango juu ya uandaaji wa bajeti kuu ya serikali ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa njia ya uchambuzi na mapendekezo.

1 UTANGULIZI

Wafanyakazi ni wadau muhimu katika kujenga uchumi wa taifa. Kuna uhusiano wa karibu kati ya wafanyakazi na sekta nyingine zote katika uchumi. Kipato kinachopatikana kutoka kwa mfanyakazi aliyeajiriwa au kujiajiri kwa namna moja au nyingine kinagusa na kufika katika maeneo tofauti kwa njia ya wao kukidhi mahitaji mbalimbali ya bidhaa na huduma. Mbali na umuhimu wao mkubwa katika taifa, wafanyakazi wa sekta ya umma wamekua na mahitaji ya aina tofauti yanayohusu kupanda madaraja, nyongeza ya mishahara na malimbikizo ya aina nyingine. Ili maslahi ya wafanyakazi yaweze kuboreshwa, ufanisi wa utekelezaji wa bajeti na kuongezeka kwa mapato ya serikali kuna mchango mkubwa kwa wadau wote katika uchumi.

Mara zote nia na mwelekeo wa THTU ni daima kujenga, Taifa kwanza. Kwahiyo lengo la andiko hili la Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) ni kuweka wazi uchambuzi mfupi wa mwenendo wa mapato na matumizi, na kushauri kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, kupendekeza namna bora ya kuimarisha na kuongeza mapato ya serikali, utekelezaji wa sera ya viwanda, namna TEHAMA na mifumo ya kielektroniki inavyoweza kuboreshwa kusaidia ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa njia bora zaidi. Dhamira kubwa ni kuyafanya hayo yote kwa maslahi mapana ya taifa, kukuza uchumi ili mwisho wa siku maslahi ya wafanyakazi ambao ni nguzo muhimu yaweze kuboreshwa. Lengo la uchambuzi huu, ni kuangalia ni jinsi gani hivyo vyote vitakamilishwa kwa maslahi ya wadau wote wa bajeti ya taifa na wanufaike na bajeti hiyo wakati wa utekelezaji wake. Wadau hao ni wakulima, wafanyakazi, wafugaji, wafanyabiashara na wananchi wengine kwa ujumla.

2 MIONGOZO MIKUU YA MAANDALIZI YA BAJETI

Miongoni mwa miongozo inayotumika kutayarisha bajeti ya serikali ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2015–2020) na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21). Hivyo hata kwa mwaka wa fedha 2019/20 miongozo hii inatumika. Yafuatayo ni maelezo jinsi hii miongozo inavyotumika katika uandaaji wa bajeti ya serikali:

2.1 Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongoza harakati za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zitakazoiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Katika kuchambua bajeti kuu ya serikali Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inaangazia malengo ambayo ni

kuhakikisha kuwepo kwa jamii iliyoeleimika vema na inayojifunza na kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine. Ili kutimiza malengo hayo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuboresha viashiria muhimu vya uchumi kama vile kuchochea ukuaji wa pato la taifa, kushusha mfumuko wa bei, kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, kupunguza ukosefu wa ajira pamoja na kuendeleza sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mpango elekezi wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka 15: Mpango huu ni muhimu katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kwa kuwa umeweka wazi mwelekeo wa kimkakati kwa muda mrefu na nguzo kuu kwa umakini zaidi, uratibu na kuoanisha mipango iliyowekwa ili kuleta maendeleo. Utekelezaji wa mpango huu unafanyika katika vipindi vitatu: **kipindi cha kwanza (2011/12-2015/16)** kilihusu uboreshaji wa miundo mbinu ya usafiri, nishati na maji, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii, **kipindi cha pili (2016/17–2020/21)** kinabeba dhana ya uchumi unaotegemea viwanda; na **kipindi cha tatu (2021/22–2025/26)** kinahusu ongezeko la ushindani kuwezesha bidhaa zinazozalishwa kuuzwa nje ya nchi. Tunashauri serikali kupitia bajeti ya 2019/20 iendelee kutoa kipaumbele kwenye upatikanaji wa maji vijijini na kukiwezesha kilimo cha umwagiliaji; nishati endelevu kama umeme wa nguvu za jua na upepo; kujenga na kuimarisha miundombinu ya maghala yenye sifa ya kuhifadhi vyakula katika ubora unaostahili; kuweka uwiano mzuri kati ya aina ya viwanda vinavyoanzishwa na rasilimali watu wanaozalishwa au/na kuendelezwa na taasisi zetu za elimu na mafunzo. Ni vyema viwanda hivyo vikagusa sekta za kitaifa zinazotegemewa na watanzania wengi kama kilimo, ufugaji na uvuvi.

2.2 Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015–2020

Ilani hii iliandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mwelekeo wa Sera za CCM zenye lengo na nia ya kuendelea kuwatumikia wananchi kwa kipindi cha miaka mitano (2015-2020). Vipaumbele vya ilani ni pamoja na: ustawi wa wananchi; kuiwezesha nchi kupata mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii; kuondoa umaskini na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana. Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 iendelee kuangazia mambo muhimu yaliyopo kwenye ilani kama vile: kuongeza kasi ya kupima maeneo ya wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na kuwapatia hati miliki za kimila ambazo watazitumia kama dhamana ya kuwawezesha kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zao za kilimo, ufugaji, uvuvi na nyinginezo; kuongeza kasi ya kurasimisha biashara na kuwapatia wafanyabiashara wadogo maeneo ya kufanyia biashara, leseni na fursa za kupata mikopo yenye masharti

nafuu; na kuanzisha ajira kwa vijana kupitia sera ya viwanda vyenye fursa kubwa za ajira.

2.3 Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21) unatekelezwa kwa kufuata utaratibu wa mwaka mmoja mmoja. Mpango una malengo na vipaumbele kama ifuatavyo kufikia 2020/21: ukuaji wa uchumi (kufikia asilimia 10); mfumuko wa bei (wastani usiozidi asilimia 5); udhibiti wa ukuaji wa deni la taifa; udhibiti wa sarafu dhidi ya fedha kuu za kigeni (mfano TZS 2,185.62/1$ isizidi ifikapo mwaka 2020/21); viwango nafuu vya riba kwa sekta binafsi; urari wa biashara na ukuaji wa sekta ya kilimo.

Takwimu zinaonyesha malengo ya ukuaji wa uchumi ni asilimia 10 kufikia mwaka 2020/21. Hatua ya lengo hili mpaka sasa ni asilimia 7.1 (2016/17) na asilimia 7.2 (2017/18). Suala la majadiliano ni uhalisia wa ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi kitaifa. Ni vyema ukuaji wa uchumi wa taifa ulinganishwe na ukuaji wa kipato na maendeleo ya mwananchi wa kawaida. Watanzania wengi (zaidi ya asilimia 65) wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi. Ili utekelezaji wa awamu ya pili ya kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP II) na maeneo mengine ya kipaumbele ufanyike kwa ufanisi sekta hizi zipewe kipaumbele katika bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2019/20.

Kuhusu udhibiti wa mfumuko wa bei kubaki katika lengo kuu la wastani usiozidi asilimia 5 (ifikapo 2020/21), mfumuko wa bei kwa mwaka 2016/17 ulikuwa asilimia 5.3 na kupungua hadi asilimia 4.3 kwa mwaka 2017/18, ambapo inaonekana hali ni nzuri kwa kubakia tarakimu moja[1]. Serikali iendelee kuimarisha jitihada za kuangalia maeneo yanayosababisha mfumuko wa bei kama vile bei ya mafuta, sera za fedha na bidhaa nyingine muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kama vile chakula na madawa. Udhibiti wa mafuta kwa kufuata bei elekezi inayolingana na soko la dunia itadhibiti mfumuko wa bei. Serikali ihakikishe vyakula na madawa yanayoweza kuzalishwa na kuongezwa thamani hapa nchini vizalishwe na kuimarisha uwepo wa kutosha katika soko la ndani. Udhibiti wa sera za fedha ni muhimu ili kutunza thamani ya fedha na kuchochea ukuaji wa uchumi kama vile kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni kwa matumizi yasiyo ya lazima.

[1] Chanzo cha taarifa zote ni Wizara ya Fedha na Mipango.

Deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 39.4 ya pato la taifa kutoka Juni 2017 mpaka Juni 2018 kutokana na serikali kuendelea kukopa ili kugharamia bajeti kuu ya nchi. Serikali iangalie uwezekano kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 kuweka utaratibu wa kulipa madeni ya ndani na nje; pamoja na, madeni ya wakandarasi wa ndani, malimbikizo ya stahiki mbalimbali ya wafanyakazi wa umma. Inashauriwa ukopaji utakaofanyika kwa mwaka wa fedha 2019/20 uwe kwa ajili ya miradi ya maendeleo na inayoleta tija kwa taifa.

Takwimu zinaonyesha viwango vya riba vinaimarika japo taasisi nyingi za kifedha zinakopesha zaidi sekta binafsi zinazojihusisha na biashara; na kwa kiwango kidogo kwenye uwekezaji wa viwanda huku sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi zinazoajiri watanzania wengi zikikosa huduma za kifedha na mikopo kwa kiasi kinachoridhisha. Ili kuwezesha ukuaji wa sekta binafsi na uwekezaji, bajeti ya 2019/20 iangazie kujenga mazingira rafiki ya kufanya biashara na kuwezesha upatikanaji wa ajira mpya kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21). Pia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 ihakikishe wafanyakazi walioajiriwa na waliojiajiri katika sekta binafsi wanapewa mazingira ya uhakika wa ajira na biashara zao. Ili kuimarisha shughuli zao hizo za kiuchumi, maazimio yanayotokana na mazungumzo ya kisera kati ya serikali na wadau wote, ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na vyama vya wafanyakazi yawe yanatekelezwa kwa kipindi walichokubaliana.

3 MWENENDO WA BAJETI YA TAIFA

3.1 Mchakato na Vipaumbele vya Bajeti

Bajeti ya taifa huwa inaandaliwa na kuwasilishwa kabla ya kila mwaka wa fedha mpya kuanza. Katika kuandaa bajeti ya mapato na matumizi ya serikali, sera au miongozo mbalimbali hutumika; vipaumbele hutolewa na serikali, ambavyo vinatazamiwa katika uandaaji wa bajeti hiyo. Mwenendo wa bajeti iliyopita na inayopendekezwa pia hutolewa. Vyanzo vya mapato vya zamani huboreshwa na vipya hupendekezwa ambavyo vitatumika kutekeleza bajeti hiyo. Pia matumizi pendekezwa hujadiliwa na kupitishwa ili bajeti ianze kutumika.

Mchakato wa maandalizi ya bajeti unahusisha taasisi zote za umma ikiwemo mihimili ya dola. Maandalizi hayo ya bajeti yanategemea miongozo mingi inayogusa sera, sheria, dira, ilani ya chama (CCM), mikakati na programu mbalimbali za kitaifa zinazoungwa mkono na taasisi husika.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 yameainisha maeneo ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa bajeti. Maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17–2020/21 na Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango huo. Maeneo hayo ni:

1) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa misingi ya uchumi wa viwanda,
2) Ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji,
3) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, na
4) Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mpango.

3.2 Sera, Mwenendo na Tathmini ya Bajeti

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 serikali imefanya juhudi katika kutafuta mbinu mbadala za kuongeza na kuimarisha mazingira ya kukusanya pato la ndani. Juhudi hizi zinajumuisha kufanya marejeo ya baadhi ya sheria za kodi ili ziweze kuendana na mazingira ya nchi yaliyopo. Malengo makuu ya kisera katika kuongeza makusanyo ya mapato ni pamoja na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija, kuongeza utumiaji wa mifumo ya kielektroniki katika ukusaji wa mapato, kuendelea kuboresha usimamizi na ukaguzi kwenye mipaka ya nchi, bandari na viwanja vya ndege, na kupanua wigo wa mapato. Sanjari na hilo, serikali imekua ikiweka vipaumbele katika kuongeza ufanisi wa matumizi ya mapato, miongoni mwa vipaumbele hivyo ni pamoja na kudhibiti ongezeko la malimbikizo ya stahiki za wafanyakazi pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Ufanisi wa makusanyo upande wa Serikali za Mitaa umekua duni, kwa mfano kwa wastani wa kipindi miaka mitatu iliyopita ni asilimia 79 tu ya makusanyo yalipatikana ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Juhudi kwenye kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato, urasimishaji wa sekta zisizo rasmi, kuimarisha taasisi husika na kuwezesha mazingira rafiki ya uwekezaji na uanzishwaji wa viwanda na kuongeza wigo na usimamizi wa makusanyo yatokanayo na kodi za mifugo, nyumba, ardhi na maliasili nyingine kama misitu, madini, utalii, gesi asilia na samaki bado unahitajika.

Malipo ya mishahara ya wafanyakazi pia yamekua hayafikii malengo (Jedwali Na. 1 na Kielelezo Na. 1). Kutofikia lengo la bajeti eneo hili kunaibua malimbikizo mapya yasiyo ya lazima. Sanjari na hilo, mabadiliko ya masharti na gharama za mikopo ya nje na kuongezeka kwa deni la taifa kunatoa tafsiri ya kuhitajika kwa umakini na kuongeza juhudi ya kupata vyanzo nafuu na rafiki zaidi vya mapato hasa vya ndani.

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Bajeti kuanzia 2015/16 mpaka 2018/19

Na.	Eneo	Mwaka wa Fedha			
		2015/16	**2016/17**	**2017/18**	**2018/19**
Mpango wa Bajeti/Mapato (TZS)					
1a.	Jumla ya bajeti	22.49 tril	29.54 tril	31.71 tril	32.48 tril
2a.	Vyanzo vya ndani	13.99 tril	18.46 tril	19.98 tril	20.89 tril
3a.	Vyanzo vya nje	8.5 tril	11.08 tril	11.73 tril	11.59 tril
4a.	Matumizi ya kawaida	16.57 tril	17.72 tril	19.71 tril	20.47 tril
5a.	Matumizi ya maendeleo	5.91 tril	11.82 tril	11.99 tril	12.01 tril
Matumizi Halisi (Julai mpaka Aprili) (TZS)					
1b.	Jumla ya matumizi	16.86 tril	25.42 tril	21.68 tril	
2b.	Vyanzo vya ndani	11.48 tril	16.64 tril	14.84 tril	
3b.	Vyanzo vya nje	5.38 tril	8.78 tril	7.84 tril	
4b.	Matumizi ya kawaida	13.65 tril	18.14 tril	16.56 tril	
5b.	Matumizi ya maendeleo	3.21 tril	7.27 tril	5.12 tril	
Bajeti za Kisekta (TZS)					
6.	Kilimo, ufugaji & uvuvi	1.00 tril	1.06 tril	1.04 tril	
7.	Miradi ya miundombinu	2.43 tril	5.47 tril	5.54 tril	
8.	Umeme	0.92 tril	1.13 tril	0.99 tril	
9.	Elimu	3.87 tril	4.77 tril	4.71 tril	
10.	Afya	1.82 tril	1.99 tril	2.22 tril	
11.	Maji	0.57 tril	1.02 tril	0.75 tril	
Bajeti na Malipo ya Mishahara na Malimbikizo (TZS)					
12.	Bajeti ya mishahara	6.5 tril	6.6 tril	7.21 tril	7.41 tril
13.	Malipo ya mishahara	5.6 tril	5.6 tril	6.3 tril	
14.	Malipo ya Malimbikizo	1.13 tril		1.17 tril	
Deni la Taifa (mpaka Aprili ya mwaka husika) (TZS)					
15.	Jumla ya kiasi cha deni	$20.94 bil	43.79 tril	49.65 tril	

N.B: Taarifa za mwaka wa fedha 2018/19 ni kwa viwango vilivyopatikana kwenye bajeti.

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, serikali imeainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyotazamiwa kugharimia shughuli za maendeleo. Jumla ya TZS trilioni 12.38 sawa na asilimia 37 ya bajeti yote inapendekezwa kutumika katika miradi ya maendeleo. Hata hivyo mwenendo wa upatikanaji wa mapato ya utekelezaji wa bajeti unatia shaka katika kufikia lengo

lililokusudiwa. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 kati ya TZS trilioni 11.8 zilizotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo ni kiasi cha TZS trilioni 6.4 tu sawa na asilimia 55 ndicho kilipatikana katika kutekeleza lengo. Vivyo hivyo, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ambapo kati ya TZS trilioni 11.4 ni TZS trilioni 6.5 pekee sawa na asilimia 57 zilitolewa. Hali hii ya kushindwa kutekelezeka kwa malengo ya mpango wa maendeleo inatokana na ukusanyaji hafifu wa mapato ya ndani na utegemezi wa fedha za mikopo na fedha za wafadhili kutoka kwa wahisani.

Kielelezo Na. 1: Uhusiano wa Bejeti na Malipo Halisi ya Mishahara



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3 Vipaumbele Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20

Katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, sekta zilizopewa kipaumbele ni pamoja na miradi ya umeme inayotumia mfumo wa maji, ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa, barabara na ukuaji wa sekta ya anga. Lengo kuu ni kurahisisha na kuhamasisha ukuaji wa sekta ya utalii hasa nje ya mipaka ya Tanzania.

Ingawa katika bajeti ya mwaka 2019/20 serikali imeweka mkazo katika kuboresha miundombinu itakayovutia uwekezaji nchini, suala la kutoweka vipaumbele katika sekta za huduma za kijamii pamoja na kilimo zinatia shaka juu ya hatua madhubuti zinazochukuliwa katika kuboresha maisha ya watu, wakiwemo wakulima na wafanyakazi.

3.3.1 Kilimo, Ufugaji na Uvuvi

Kwa mujibu wa maelezo ya serikali katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, sekta ya kilimo imepewa kipaumbele katika ukuaji wake. Hata hivyo, katika sekta tano zilizoainishwa, sekta ya kilimo haimo, jambo ambalo linatilia shaka mkazo wa serikali katika kuchukua hatua madhubuti za kukuza sekta hii ambayo ndio imeajiri watanzania wengi na sekta muhimu katika maendeleo ya viwanda. Ikumbukwe utekelezaji huo uko chini ya kiwango na makubaliano ya Maputo ya mwaka 2003. Umaskini na ukosefu wa ajira bado vinaacha maswali juu ya uhusiano wa kukua kwa uchumi na kuboresha maendeleo ya watu. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanyika, kiwango cha umaskini kimepungua kwa wananchi kufikia asilimia 26.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 28.2 mwaka 2012. Ingawa kiwango cha umaskini kimepungua, bado kasi ya ukuaji wa uchumi hailingani na kasi ya kuboresha maisha ya watanzania. Hii inatokana na ukweli kwamba, sekta nyingi zinazochangia pato la taifa kwa kiwango kikubwa hazitoi ajira ya moja kwa moja kwa wananchi. Mikakati thabiti ya kuendelea kuboresha sekta ya kilimo ambayo inatoa ajira kwa zaidi ya nusu ya watanzania inahitajika.

3.3.2 Viwanda, Biashara na Uwekezaji

Ni wazi kwamba serikali ya awamu ya tano imejipambanua katika kuwekeza nguvu zake nyingi katika kujenga uchumi wa viwanda. Hata hivyo, Tanzania imekuwa haifanyi vizuri katika kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara ikiwemo kuvutia wawekezaji. Kwa mfano, ripoti ya Benki ya Dunia, "*Doing Business Report 2019*", Tanzania inashika nafasi ya 144 kati ya nchi 190 ikiporomoka kwa nafasi 7 kutoka 137 kwa mwaka 2018. Maeneo ambayo bado yamekuwa hayafanyi vizuri ni pamoja na kufanya biashara nje ya mipaka ya nchi, ukwepaji wa kodi kwa wawekezaji, upatikanaji wa vibali vya kuanzisha na kufanya biashara, ucheleweshaji wa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya viwanda, uandaaji wa miundombinu wezeshi itakayosaidia wawekezaji kufanya kazi zao vizuri (uwepo wa umeme wa kutosha na wa uhakika, maji na barabara) na namna bora ya kuwalinda wawekezaji.

3.3.3 Miradi ya Miundombinu

Serikali imefanikiwa kufufua shirika la ndege, kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu barabara na kuanza ujenzi wa reli ya kisasa. Hata hivyo, maboresho na maendeleo ya ujenzi wa miundombinu bado haujaweza kuwiana na nia ya serikali katika kuvutia wawekezaji wengi kuja nchini. Licha ya kwamba serikali imeboresha na kuongeza upatikanaji wa umeme viwandani gharama za uzalishaji na upatikanaji wake upo juu, huku kwa baadhi ya maeneo umeme si wa kutosha na uhakika kwa wananchi na wawekezaji kuendesha shughuli zao. Katika bajeti inayopendekezwa ya mwaka wa

fedha 2019/20, ni muhimu serikali ikaharakisha mradi wa upatikanaji wa umeme wa Stiegler's Gorge utakaosaidia ukuaji wa sekta ya viwanda na uwekezaji.

4 MAPENDEKEZO YA UBORESHAJI WA BAJETI YA TAIFA

4.1 Utekelezaji wa Sera ya Viwanda

Katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na nia ya kufikia uchumi wa kati, serikali imeweka mkazo mkubwa zaidi katika sera ya viwanda. Hata hivyo, takwimu zinaonesha uzalishaji wa bidhaa za viwanda haujatengamaa. Juhudi za kuimarisha uzalishaji wa viwanda ni muhimu katika kutekeleza sera za viwanda na kuongeza mauzo ya bidhaa za viwanda ndani na nje ya nchi. Jedwali Na. 2 linaonesha takwimu za mauzo ya bidhaa za viwanda nje ya nchi.

Jedwali Na. 2: Mauzo Nje ya Bidhaa za Viwanda (Katika Milioni USD)

Mwaka	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Mauzo	1,037.34	1,072.07	1,239.60	1,364.50	1,092.10	819.60

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Takwimu hizi zinaonesha kuwa, juhudi kubwa zinatakiwa katika uongezaji wa thamani wa bidhaa na kutekeleza sera ya viwanda kuelekea uchumi wa kati. Kuimarika kwa uzalishaji katika viwanda una manufaa ya moja kwa moja kwa serikali, mfanyakazi na sekta nyingine za kiuchumi na kuweza kusaidia yafuatayo:

i) Serikali itapata mapato mengi zaidi yatakayowezesha kulipa stahiki mbalimbali za wafanyakazi. Pia, serikali itapata fedha za kigeni kutokana na kuuza bidhaa za viwanda nje ya nchi zilizoongezewa thamani zaidi.
ii) Kuwepo kwa bidhaa nyingi zizalishwazo viwandani hasa zinazotegemea malighafi ya kilimo, mifugo na uvuvi; itasaidia kupunguza mfumuko wa bei na pia kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa mfanyakazi.
iii) Kuchochea ukuaji wa sekta zinazotegemewa na viwanda kama vyanzo vya malighafi, na chanzo cha ajira mpya, kwa mfano, sekta ya kilimo na ufugaji.
iv) Kupunguza utegemezi wa kupata bidhaa kutoka nje ya nchi kwa sababu bidhaa hizo zitakuwa zinazalishwa ndani ya nchi. Hii itaimarisha thamani ya fedha ya ndani na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.
v) Kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi. Hii itachochea ukuaji wa uchumi, ujuzi na teknolojia.

Ufanisi wa utekelezaji wa sera ya viwanda utasaidia sana kuongeza mapato ya serikali na hivyo kuiwezesha kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Ili kufikia ufanisi huo, lazima

kuwe na namna bora zaidi ya kutekeleza sera ya viwanda. THTU inapendekeza yafuatayo:

i) Serikali ielekeze nguvu katika kuchochea viwanda vinavyotumia malighafi nyingi za ndani zinazotokana na mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii itachochea uzalishaji wa ndani, kukuza kipato cha wazalishaji wa malighafi hizo na kukuza pato la taifa.
ii) Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali (wawekezaji, sekta za umeme na maji, usafirishaji n.k) katika maamuzi na uandaaji wa miongozo mbalimbali inayohusiana na sera ya viwanda. Hii itasaidia kuwa na dhamira ya pamoja katika utekelezaji wa sera ya viwanda.
iii) Kuimarisha sekta za kilimo, uvuvi na ufugaji. Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 ielekeze nguvu katika kuimarisha miundombinu na masoko ya mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Hii itachochea upatikanaji wa malighafi nyingi muhimu kwa viwanda.
iv) Kujenga kiwanda kikubwa cha kisasa cha kubangua korosho ili kuongeza thamani ya bidhaa za korosho, kukuza ajira na kuongeza ukusanyaji wa mapato.
v) Kuvijengea uwezo zaidi vituo na vyuo vya ufundi stadi vya juu, kati na vidogo ili kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vitakavyo chochea ukuaji wa pato la taifa.
vi) Kuongeza kasi ya uimarishaji wa masoko na miundombinu hasa ya barabara vijijini ili kuchochea biashara, uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo; sekta ambayo inategemewa na asilimia kubwa ya watanzania waishio vijijini na pia viwanda vingi vidogo, vya kati na vikubwa kama chanzo cha malighafi.

4.2 Uimarishaji wa Mapato Kuongeza Uwezo wa Serikali

Ili kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, sera za mapato kwa mwaka wa fedha 2019/20 zijikite katika kuongeza na kuboresha vitu vifuatavyo:

1) Wigo wa kodi, na ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato,
2) Kuimarisha usimamizi wa vyanzo vilivyopo hususan katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki na hatua nyingine za kiutawala, na
3) Kupunguza matumizi yasiyo na tija.

Maeneo muhimu ambayo serikali inashauriwa izidi kuangazia katika kuongeza mapato (uwepo wa mbinu bunifu, rafiki, shirikishi na za kimkakati), kama ifuatavyo:-

1. Kuendelea kurasimisha sekta zisizo rasmi na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata vyanzo vipya vya mapato, mfano uthaminishaji wa majengo na

kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi, kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo kama Machinga, wavuvi, shughuli za ufundi (ujenzi, useremala, uchomeleaji, washonaji nk)na mama lishe. Wachomaji wa nyimbo kwenye CD na flash ili kulinda kazi za wasanii nao usishaulike katika kutozwa kodi.Mifumo ya kielektroniki itasaidia kuwatambua na kutengeneza utaratibu rafiki wa kutoza kodi.

2. Michezo ya kamari na kubahatisha kuongezewa kiwango cha kodi. Tunapendekeza ongezeko la kutoka asilimia 18 hadi 30 (serikali ya Kenya yenyewe inatoza asilimia 35) ya pato ghafi, hii itasaidia pia kuondoa urahibu kwa vijana na kuelekeza nguvu kwenye shughuli zingine za kimaendeleo.
3. Misamaha ya kodi itathiminiwe, isiyo na tija ipunguzwe zaidi ili kuongeza makusanyo ya serikali, tunatambua umuhimu wa misamaha ya kodi katika kuchochea maendeleo hasa maendeleo ya jamii na uwekezaji. Lakini pia wanufaikaji wanatumia vibaya misamaha hiyo kwa maslahi binafsi na kuipotezea serikali mapato. Tunashauri kuwepo na umakini na ufuatiliaji wa kina kwenye misamaha hiyo, ili itumike kama ilivyokusudiwa na sio kutumika kwa manufaa binafsi. Ikumbukwe Tanzania imeonekana ina misahama ya kodi mingi kuliko nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki.
4. Kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi. Sheria yetu ya kodi ya mapato (Income Tax Act) na sheria nyingine za kodi ziendelee kuboreshwa ili kusaidia kupunguza mianya ya ukwepaji kodi (Tax avoidance). Pia tunashauri serikali izidi kuboresha mifumo ya ukusanyaji kodi na hasa kutumia teknolojia za kielektroniki kupunguza wakwepa kodi, ambao Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inashindwa kuwafikia au kupata taarifa zao kwa usahihi.
5. Tunashauri TRA ichukue hatua za makusudi za kuboresha mahusiano kati yake na walipa kodi (to increase voluntary tax compliance) kwa lengo la kuondoa dhana iliojengeka miongoni mwa walipa kodi kuwa TRA inatumia nguvu na vitisho kudai kodi na hivyo kuzorotesha ukusanyaji wa mapato.
6. Kupunguza changamoto zinazohusiana na mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji nchini. Kupungua kwa changamoto hizi kutachangia kukuza biashara zilizopo (kukuza mitaji) na pia kuvutia wawekezaji wapya na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya serikali. Baadhi ya changamoto ambazo zinapaswa kumulikwa zaidi ni hizi zifuatazo:
    6.1. Migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali za serikali,

6.2. Gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na utitiri wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu ngumu na nyingi zenye urasimu usio na tija na hivyo kutoa mianya na mazingira ya rushwa,

6.3. Muingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

7. Ofisi ya Msajili wa Hazina iimarishe usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo serikali ina hisa ili kuhakikisha kuwa gawio stahiki katika uwekezaji wake linapatikana.
8. Mamlaka za Serikali za Mitaa zijielekeze kwenye miradi itakayochochea upatikanaji wa mapato katika mamlaka hizo hususan viwanda, minada ya mifugo, masoko na machinjio ya kisasa, stendi za mabasi, stendi za maegesho ya malori, ushuru wa mazao na maghala ya kuhifadhia nafaka. Utekelezaji wa haya utapunguza utegemezi kwa serikali kuu.
9. Tunashauri Maafisa Masuhuli wazidi kusisitizwa kutumia wakandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki za kukusanya mapato na ambao wanakumbukumbu safi za kulipa kodi kutoka TRA. Pia uwepo wa utaratibu mzuri kwa wafanyabiashara wadogo kwa kuwawekea kodi ya zuio wanapotoa huduma kwa taasisi za serikali ni muhimu.
10. Kuongeza kasi ya ufuatiliaji, utambuzi wa wamiliki na kuweka utaratibu mzuri wa kukusanya kodi ya zuio inayotokana na ukodishaji wa ardhi na majengo. Kodi hii iliyosahaulika inakadiriwa kuongeza mapato kwa kiasi kisichopungua TZS Bilioni 400.
11. Pia tunapendekeza sheria ya madini iangaliwe vizuri ili kodi stahiki ya serikali iweze kukusanywa. Uwepo wa mfumo imara na sahihi wa kukusanya kodi ya madini utasaidia.
12. Matumizi yakinifu ya TEHAMA katika sekta ya utalii yanaweza kuongeza tija na mapato. Ili kuongeza tija katika sekta ya utalii kupitia TEHAMA, tunapendekeza kuongeza muonekano “visibility” ya vivutio vya kitalii kupitia mitandao. Sambamba na hilo, juhudi ziongezwe katika kuongeza upatikanaji wa maudhui ya ndani zinazoweza kuitangaza Tanzania kimataifa na hatimaye kuongeza mapato ya utalii.
13. Matumizi ya kimkakati ya TEHAMA yanaweza kuchochea tija katika sekta ya kilimo. Yafuatayo ni mapendekezo ya namna TEHAMA inavyoweza kuchochea tija kwa wakulima.

13.1. Kuboresha uratibu wa mifumo ya taarifa mbalimbali ikiwemo masoko, bei, hali ya hewa na pembejeo kwa wakulima kupitia mifumo ya kielektroniki.

13.2. Kutumia mifumo ya TEHAMA kuboresha upatikaji wa pembejeo zenye ubora unaokubalika kwa ajili ya matokeo bora ya uzalishaji.

13.3. Uanzishwaji wa minada ya mazao kupitia majukwaa rasmi ya kielektroniki (e-auctions platforms). Hii itaongeza wigo, ushindani na uwazi katika ununuzi wa mazao ya kilimo na mifugo na kuongeza kodi inayopatikana na sekta ya kilimo na mifugo.

13.4. Kutumia mifumo ya kielektroniki katika kuboresha miundombinu ya masoko na maghala bora ya kuhifadhia mazao mbalimbali na kuanzisha stakabadhi za kielektroniki ya mazao ghalani. Hii itasaidia kuwawezesha wakulima kuwa na ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kukidhi vigezo vya kukopesheka.Vile vile uwepo wa mifumo madhubuti ya taarifa kuhusiana na mazao na maghala. Hili litavijengea vyama vya ushirika uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ndani na nje.

14. Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatokanayo na usambazaji wa huduma za maji.

15. Kuboresha makusanyo na usimamizi wa mapato na matumizi katika sekta ya afya. Katika eneo hili, yafuatayo yanapendekezwa:

15.1. Juhudi zaidi zilekezwe kwenye kuziunganisha hospitali na vituo vya afya katika kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma za afya. Hospitali nyingi ziunganishwe na mfumo wa GOT-HOMIS.

15.2. Usimamizi wa mnyororo wa usambazaji wa madawa uzingatie matumizi madhubuti ya TEHAMA ili kupunguza upotevu wa madawa na kuboresha upatikanaji wa dawa na uandaaji wa maoteo sahihi ya madawa yanayotolewa kwa hospitali za umma kuliko ilivyo sasa.

16. Katika sekta ya madini, tunapendekeza maboresho ya upatikanaji wa taarifa za masoko na bei za madini. Hii itasaidia ushindani wa sekta ya madini kitaifa na kimataifa. Tunapendekeza uwepo jukwaa rasmi la TEHAMA litakalotoa taarifa hizi muhimu kwa wadau wa sekta ya madini.

4.3 Maboresho ya Mifumo ya Kukusanya Kodi

Eneo la mifumo inayosaidia kuongeza ufanisi wa kukusanya mapato ya aina tofauti ya serikali limeonekana linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kutokuwepo kwa mifumo thabiti yenye ufanisi kwenye ngazi zote. Pamoja na juhudi za sasa za ukusanyaji na usimamizi wa mapato, bado uboreshaji unapaswa kuendelezwa kutokana na changamoto za kukua kwa teknolojia. Taarifa mbalimbali kupitia hotuba

za bajeti zimethibitisha hilo. Matumizi mazuri ya TEHAMA na mifumo ya kielektroniki ya kumtambua mlipa kodi na kukusanya mapato limeonekana ni jambo muhimu. Yafuatayo ni mapendekezo ya kimkakati juu ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo ya kielektroniki ya mapato, hatimaye kusaidia katika ukusanyaji wa mapato kwa njia bora zaidi kuliko ilivyo sasa:

1. Uboreshaji wa mbinu za ulinzi wa mifumo ya huduma mbalimbali zinazohusiana na ukusanyaji wa kodi ili kupambana na uhalifu wa kimtandao unaoweza kuathiri ukusanyaji na upatikanaji wa taarifa sahihi za mapato. Ripoti ya shirikisho la mawasiliano la kimataifa (ITU) ya mwaka 2017 kuhusiana na usalama wa kimtandao (Cyber Security Index) imeorodhesha Tanzania kuwa ni miongoni mwa nchi zisizo na na usalama wa kuridhisha kimtandao. Ripoti ya kampuni kubwa ya programu za kompyuta duniani ya Microsoft, inabainisha Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizo katika hatari kubwa zaidi duniani ya mashambulizi ya kimtandao na udukuzi wa kiteknolojia.

   Aidha, ripoti ya uhalifu wa kimtandao ya mwaka 2016 ya shirika lisilo la kiserikali la SERIANU inaonesha Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa kupoteza fedha nyingi kupitia uhalifu wa kimtandao. Ripoti hiyo inaonesha Tanzania imepoteza takribani TZS bilioni 187 (Dola za kimarekani milioni 85) kutokana na uhalifu wa kimtandao. Katika ripoti hiyo taasisi za kibenki zimeorodheshwa kama wahanga wakubwa wa uhalifu huu. Pamoja na juhudi za sasa za serikali kupitisha sheria ya uhalifu mtandaoni (Cybercrime Act 2015) na mapitio ya sera ya taifa ya TEHAMA, juhudi madhubuti zinapaswa kuwekezwa katika kuongeza rasilimali watu katika sekta ya usalama wa kimtandao na ubora wa miundo mbinu ya TEHAMA katika ngazi zote.

2. Kuboresha mfumo tangamani wa matumizi (framework of adoption) ya TEHAMA katika serikali ili kuwa na ufanisi wa kuiboresha, kuikagua na kuunganisha. Uboreshaji huo utasaidia kupunguza hatari za uvamizi wa kimtandao na udukuzi. Kwa hali ya sasa mifumo mingi haijaunganishwa kufanya kazi pamoja na mifumo mingine ya serikali kutokana na makusudio ya uundwaji wake na miundo yake kiteknolojia. Hii ni changamoto inayokabili mifumo mingi ya kielektroniki ya huduma (e-sevices) kutokana na ukosekanaji wa viwango vya kitaifa na kimataifa, mfano namba msimbo za huduma (service codes).

Ukosekanaji wa mahusiano kati ya mifumo mbalimbali, mbali na kuongeza gharama za utendaji wake pia unaathiri tija ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa taarifa sahihi za mifumo tofauti inayoingiliana. Kupitia wakala wa serikali mtandao na taasisi za tafiti, juhudi za pamoja ziongezwe katika kutengeneza kanuni na viwango vya ubora wa mifumo ya TEHAMA inayotumika serikalini. Hali kadhalika, juhudi zielekezwe katika kujenga uwezo wa ndani katika kuunda na kuratibu mifumo ya serikali hasa inayohusiana na mapato. Hii itapunguza gharama kubwa zinazolipwa na serikali kwa makampuni ya kigeni katika kununua mifumo ya TEHAMA na ushauri wa kitaalamu. Uwezo wa ndani, mbali na kuwa na ufanisi mkubwa ni fursa ya ajira kwa wataalamu wazalendo.

3. Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mifumo ya TEHAMA inayohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa kodi. Hii itasaidia uhakiki wa mapema wa ubora wa mifumo hiyo na kuibua mianya ya udukuzi na udanganyifu inayoweza kutokea kutokana na ukuaji wa teknolojia. Hali kadhalika, mapitio ya mara kwa mara yatasaidia mifumo hiyo kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

4. Kuweka mikakati ya kuboresha kanzidata ya huduma, bidhaa sanjari na taarifa za walipa kodi. Mfano taarifa za majengo, ununuzi na umiliki wa ardhi, matangazo ya biashara, leseni mbalimbali n.k. Mikakati hii iende sambamba na kurasimisha namba msimbo za huduma mbalimbali (service codes) ili kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa (data sharing) kati ya mifumo mbalimbali ya huduma ili kuongeza ufanisi. Aidha uunganishwaji wa mifumo hii utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa wakati na kuweza kutumiwa na wadau tofauti ili kurahisisha ufuatiliaji, utambuzi na utoaji wa msaada hasa kwa walengwa kwenye jamii, biashara, uwekezaji, viwanda n.k.

5. Katika kuongeza usimamizi na ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato, matumizi madhubuti ya TEHAMA katika kutengeneza ramani za kidigitali zitakazosaidia serikali kuimarisha viwango vya ukusanyaji mapato na kutoa maelezo ya biashara zote na majengo ambayo yanapasa kulipiwa ada mbalimbali ikiwemo ile ya ardhi. Kwa ujumla wake matumizi hayaya teknolojia hususani TEHAMA yatawezesha takwimu kupatikana kwa urahisi na hivyo kurahisisha kuongeza ufanisi wa mipango mikakati ya maendeleo.

6. Kuongeza upatikanaji wa huduma za serikali mtandao (e-service) hususani huduma za kikodi ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza tija kwa wateja wa huduma hizo. Mfano, huduma ya upatikanaji wa leseni za biashara, taarifa za kodi kwa mteja mmoja mmoja (Tax information dashboard). Vile vile mikakati ielekezwe kwenye kuunganisha taarifa mbalimbali za walipa kodi ili kurahisisha utambuzi na ufuatiliaji wa walipa kodi.

7. Mamlaka ya kodi na taasisi nyingine za serikali zinazohusika na ukusanyaji wa tozo na ada mbalimbali zinapaswa kuhakikisha mchakato wa malipo unakuwa rafiki kuanzia usajili hadi malipo. Aidha, mifumo ya kodi inapaswa kuwa rafiki kwa namna ambayo itaruhusu walipa kodi kujikadiria (self assessment) ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa taarifa zao za kodi. Kwa mfano, taarifa kwa wadau kuhusu ukomo wa tozo, ada, kodi n.k. Taarifa hizo zinaweza kupatikana muda wowote au kutumwa kwa mhusika kwa njia ya ujumbe mfupi, kwa mfano wiki mbili kabla ya ukomo wa uhalali wa malipo hayo kufikia.

8. Kuweka mikakati ya kuwezesha taasisi za umma kujiunga na mfumo wa malipo serikalini (GePG). Mikakati hii ni pamoja na kuzijengea uwezo wa rasilimali watu na rasilimali vifaa katika kuhakikisha taasisi hizi zinajiunga na mfumo huo kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa taarifa za makusanyo. Aidha, katika kuboresha matumizi ya GePG na mifumo mingine ya TEHAMA katika ukusanyaji na usimamizi wa kodi, ni sharti kuboresha ufanisi na upatikanaji wa miundombinu ya TEHAMA serikalini kwa ujumla. Tunapendekeza uwepo wa utaratibu maalumu wa kisera wa punguzo la kodi kwa vifaa wezeshi vya miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi za umma. Hii itaongeza motisha na kuchochea kasi katika matumizi ya TEHAMA yenye viwango katika taasisi za umma.

9. Tunapendekeza kuongeza kasi ya matumizi ya stempu za kodi za kielektroniki (Electronic Tax Stamp - ETS) kwa bidhaa zote nchini. Mfumo huo wa stempu za kodi za kielektroniki utaiwezesha serikali kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi za uzalishaji wa bidhaa za viwanda na kwa wakati. Pia mfumo huu mpya utaiwezesha serikali kudhibiti uvujaji wa mapato na kutambua mapema kiasi cha kodi ya ushuru wa bidhaa, kodi ya mapato na ile ya ongezeko la thamani (VAT) itakayolipwa.

Aidha, mfumo wa stempu za kodi za kielektroniki utadhibiti tatizo la uwepo wa stempu za karatasi za kughushi ambazo zinachangia uwepo wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na zinazoweza kuathiri afya za binadamu. Mfumo huu mpya unatumika katika nchi nyingine ikiwa pamoja na Kenya, Morocco, Uturuki, Malaysia, Afrika Kusini na Uswisi na umekuwa na mafanikio makubwa. Pia kutiliwe mkazo kwenye stempu za mikataba ambapo uzoefu unaonyesha mikataba mingi haiwekwi wazi ili stampu zitakazowekwa ziakisi thamani halisi ya mkataba. Ikiwezekana tozo kwenye mikataba ipungue ili kuhamasisha watu kuweka wazi mikataba hiyo na serikali kupata mapato.

10. Kuongeza ufanisi na juhudi katika uenezaji wa elimu ya mlipa kodi na kuongeza uelewa wa kodi kwa wananchi wote, hii itaongeza utayari na hamasa ya kupenda kulipa kodi bila shuruti (Voluntary Tax Compliance). Matumizi bora ya TEHAMA yanaweza kusaidia kueneza elimu ya mlipa kodi kwa haraka kuliko ilivyo sasa. Mfano, kutuma ujumbe mfupi kwa kutumia simu za mkononi na matumizi ya mitandao ya kijamii.

4.4 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maslahi ya Wafanyakazi

4.4.1 Ukuaji wa Uchumi na Maslahi ya Wafanyakazi

Maudhui ya Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ni kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Hii inajumuisha mifumo miwili yaani ukuzaji uchumi (FYDP I) na kupunguza umaskini (MKUKUTA II). Baadhi ya malengo ya mpango huu yanalenga katika kuharakisha ukuaji wa uchumi na jumuishi wenye kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kunufaisha watu wengi kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji, nafasi za kazi na kuongeza ubora wa maisha kwa watu.

Katika utekelezaji wa malengo hayo, serikali imeendelea kuahidi namna nzuri ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kulingana na uwezo wa mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kumudu gharama za maisha. Maeneo ambayo yamekuwa yakitiliwa mkazo ni pamoja na ongezeko la mshahara hasa kima cha chini, kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwenye mishahara, malipo ya mshahara kwa wakati, kuwapandisha vyeo watumishi, kulipa malimbikizo ya mdai ya watumishi na kuhakikisha watumishi wanalipwa mafao yao mara baada ya kustaafu.

Hata hivyo, suala la kuboresha maslahi ya watumishi halijafanyika na kupewa uzito unaostahili katika bajeti za serikali hivyo kuwafanya watumishi kufanya kazi katika mazingira magumu na kuishi maisha yasiyo na staha na kuathiri utendaji wao wa kazi.

Suala la upandishwaji wa madaraja, nyongeza ya mwaka ya mshahara na malipo ya posho kwa watumishi limekuwa gumu kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, hivyo kuchangia malalamiko kutokana na ulimbikizwaji wa madai ya wafanyakazi na kuwafanya wabakie katika kipato au madaraja yaleyale kwa muda mrefu.

Ni vizuri ikafahamika kwamba, mfanyakazi si tu rafiki wa watu wote lakini ni kiungo muhimu katika ukuaji wa sekta zote za kiuchumi, kijamii, kisiasa na nyingine. Hii ni sawa na kusema kwamba, mfanyakazi akilipwa mshahara na malipo mengine haishii mfukoni mwake. Anacholipwa mfanyakazi huishia kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali kutoka viwandani, mashambani, ufugaji, uvuvi na kadhalika. Pia mfanyakazi hushiriki kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii, kidini, kiserikali na vikundi ambavyo mwisho wa siku pesa aliyolipwa inamnufaisha kila mtu katika nchi. Inaweza ikaelezwa mahususi kwamba, kuzingatia maslahi ya mfanyakazi ni kuliwezesha taifa katika maendeleo endelevu kwa sababu zifuatazo:

a. Kodi inayotokana na mishahara (PAYE) ni chanzo kikubwa na imara kwenye vyanzo vya mapato ya serikali
b. Wafanyakazi husaidia uwepo wa mzunguko wa pesa halali katika soko kwa kununua bidhaa na huduma,
c. Morali ya wafanyakazi ikiongezeka, ufanisi wa kazi unaongezeka na hivyo kufikia malengo tarajiwa,
d. Kuchochea ukuaji wa uchumi na ufanisi wa wadau mbalimbali wa minyororo ya thamani ya bidhaa kwa sababu sekta nyingine zinategemeana kwa uwepo wa soko la bidhaa la uhakika,
e. Kuimarisha utulivu wa kisiasa kwani manung'uniko yatapungua.

4.4.2 Mapedekezo Juu ya Sheria ya Kodi

Katika bajeti ya 2019/20, tunashauri ufanyike mapitio katika viwango vya kodi vya mtu binafsi inayousiana na makato ya kodi ya mshahara (PAYE) ili kumpatia mfanyakazi unafuu wa kodi (Tax relief). Mapendekezo yamezingatia mfumo wa kodi wa nchi nyingine za Afrika Mashariki na nchi nyingine za kusini mwa jangwa la sahara. Pendekezo mahususi linalotolewa ni kupandisha kima cha chini kisichokatwa kodi kutoka TZS. 170,000 hadi TZS. 360,000 na hivyo itapunguza maumivu ya kodi kwa mfanyakazi. Tunaomba ifahamike kwamba kwa sasa hatujaliongelea suala la kupandisha kima cha chini cha mshahara kwani TUCTA imeshafanya wajibu huo ambao tunaunga mkono. Mapendekezo haya ni mahususi kwa ajili ya kuleta unafuu wa kodi kwa mfanyakazi bila kubadili viwango vya asilimia vilivyopo kwa sasa.

Jedwali Na 3 na 4 yanaonesha viwango vya kodi vya mtu binafsi, viwango vipya pendekezwa na unafuu wa kodi kwa mfanyakazi.

Jedwali Na. 3: Viwango vya Kodi ya Mapato ya Mtu Binafsi Vilivyopo

Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara)	
Kima cha chini Kilichopo	**Kiwango cha Kodi**
Mapato yasiyozidi TZS.170,000	Hakuna Kodi
Mapato yanayozidi TZS.170,000 lakini hayazidi TZS. 360,000	9% ya mapato yanayozidi TZS. 170,000
Mapato yanayozidi TZS. 360,000 lakini hayazidi TZS. 540,000	TZS.17,100 + 20% ya mapato yanayozidi TZS.360,000
Mapato yanayozidi TZS. 540,000 lakini hayazidi TZS. 720,000	TZS.53,100 + 25% ya mapato yanayozidi TZS. 540,000
Mapato yanayozidi TZS.720,000	TZS.98,100 + 30% ya mapato yanayozidi TZS. 720,000

Chanzo: Mamlaka ya Mapato (TRA)- Kodi na ushuru mbalimbali 2018/19

Jedwali Na. 4: Viwango vya Kodi ya Mapato Pendekezwa ya Mtu Binafsi

Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara)		
Kima cha Chini kinachopendekezwa	**Kiwango cha Kodi**	**Unafuu wa kodi**
Mapato yasiyozidi TZS.360,000	Hakuna Kodi	TZS. 17,100
Mapato yanayozidi TZS.360,000 lakini hayazidi TZS. 550,000	9% ya mapato yanayozidi TZS. 360,000	TZS. 53,100
Mapato yanayozidi TZS. 550,000 lakini hayazidi TZS. 730,000	TZS. 17,100 + 20% ya mapato yanayozidi TZS. 550,000	TZS. 55,100
Mapato yanayozidi TZS. 730,000 lakini hayazidi TZS. 910,000	TZS. 53,100 + 25% ya mapato yanayozidi TZS. 730,000	TZS. 62,100

Mapato yanayozidi TZS.910,000	TZS. 98,100 + 30% ya mapato yanayozidi TZS. 910,000	TZS. 98,100

4.4.3 Mapendekezo ya Mabadiliko ya Ada na Tozo Mbalimbali

Katika kupanua wigo wa ukusanyaji mapato ya serikali na kuwezesha serikali kuweza kuhudumia zaidi wananchi wake, tunashauri mabadiliko yafuatayo kwenye tozo na ada mbalimbali kama yanavyoonekana katika Jedwali Na. 5 na 6; na rejea mbalimbali zilizofanywa kwenye nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na hali ya uchumi.

Jedwali Na. 5: Mapendekezo ya mabadiliko ya ada za leseni za udereva

Leseni za Udereva	Iliyopo	Inayopendekezwa	Badiliko
Ada ya leseni	TZS. 40,000	TZS. 50,000	25%
Ada ya majaribio ya udereva	TZS. 3,000	TZS. 10,000	233%
Leseni ya muda ya udereva	TZS. 10,000	TZS. 15,000	50%

Jedwali Na. 6: Mapendekezo ya mabadiliko ya ada za michezo ya kubahatisha

Michezo ya kubahatisha	Iliyopo	Inayopendekezwa	Badiliko
Casino ya Ardhini	18% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	25% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	7%
Casino ya Mitandaoni	25% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	30% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	5%
Kodi kwenye ushindi	20% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	30% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	10%
Kodi kwenye ushindi kwenye Casino	12% kwa mapato ya Casino	15% kwa mapato ya Casino	3%

Sport betting	25% kwa pato ghafi la mauzo	30% kwa pato ghafi la mauzo	5%
SMS	25% kwa pato halisi la mauzo	30% kwa pato halisi la mauzo	5%
Slot machines	TZS. 100,000 kwa kila mashine	TZS. 120,000 kwa kila mashine	20%

4.5 Ushirikishwaji wa vyama vya Wafanyakazi katika mikakati mbalimbali

Katika kutimiza azma ya uchumi wa viwanda, inahitajika kuwa na mfumo wa utawala na uongozi ambao utatoa fursa na kudumisha mahusiaon mazuri kati ya mwajiri na wafanyakazi. Mahusiano mazuri mahala pa kazi pamoja na mambo mengine ni ushirikishwaji wa wafanyakazi kupitia vyama vya wafanyakazi ambalo ni suala muhimu katika kufikia maamuzi ya pamoja. Umoja na ushirikiano kati ya mwajiri na mwajiriwa itapelekea utendaji bora wa wafanyakazi na kuongeza uzalishaji na tija ndani ya taasisi na nchi kwa ujumla.

Tanzania ikiwa nchi mwanachama wa Shirika la kazi Duniani (ILO) imeratibisha/imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa katika kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa vyama vya wafanyakazi katika masuala yahusuyo wafanyakazi. Baadhi ya mikataba ya kimataifa iliyoratibishwa ni Uhuru wa Kujiunga na Kinga ya Haki ya Kuunda Chama wa mwaka 1948, Na. 87; Haki ya Kuunda Chama na Haki ya Kufanya Majadiliano ya Pamoja wa mwaka 1949 Na. 98.

Mikataba hiyo ya kimataifa imeratibishwa kuwa Sheria katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya Mwaka 2004; Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004, Sheria ya Majadiliano ya Utumishi wa Umma Na. 19 ya 2003. Hivyo, ifahamike kuwa kupitia sheria tajwa hapo juu, Tanzania ni miongoni mwa nchi barani Afrika zinazotoa fursa kwa wafanyakazi kushirikishwa katika kuunda nyaraka na mikakati mbalimbali kwa kupitia majadiliano ambayo yanafanyika kwa kutumia vyombo vifuatavyo, 1) majadiliano ya pamoja (collective bargaining), na 2) majadiliano yanayofanyika kupitia taasisi mbalimbali, kwa mfano Baraza la Kazi la Uchumi (LESCO), Bodi ya Ujira (Wage Board) na Kamati za Bunge. Uwepo wa mbinu hizi unawapa fursa vyama vya wafanyakazi kushiriki katika uundaji wa sera, sheria na mikataba ya hali bora sehemu za kazi.

4.5.1 Changamoto za Ushiriki wa Vyama vya Wafanyakazi

Ni wazi kwamba vyama vya wafanayakazi Tanzania vimekuwa vikipata fursa za kushirikishwa na waajiri pamoja na serikali katika majadiliano na midahalo inayohusu

masuala ya wafanyakazi. Hata hivyo, imebainika kuwa utekelezaji wa nyarakahizo (sera na sheria) unaleta changamoto kwa wafanyakazi zinapoanza kutumika kutokana na kutokuwa na sababu zifuatazo:

i. Uwakilishi kutoka kwenye vyama vya wafanyakazi kutokuwa na uwezo wa kutosha kwenye majadiliano mbalimbali yanayofanywa kati ya vyama vya wafanyakazi, waajiri na serikali.

ii. Serikali kutozingatia na kutokutekeleza kwa wakati mapendekezo yanayotolewa na wadau hasa vyama vya wafanyakazi.

4.5.2 Mapendekezo Kuboresha Ushiriki wa Vyama vya Wafanyakazi

1) Wanachama wenye utaalamu watumike kuandaa hoja na mapendekezo mbalimbali yanayohusu masuala ya watumishi na nchi.
2) Serikali ifanyie kazi kwa wakati mapendezo yanayotokana na majadiliano ya kina yenye uthibitisho wa kitalaamu.
3) Maslahi ya kima cha chini cha mshahara yawe yanatathiminiwa mara kwa mara kulingana na mwenendo wa uchumi.

4.6 Pongezi kwa Serikali

Ni wazi kuwa wafanyakazi wanatambua kazi inayofanywa na serikali katika kusukuma gurudumu la maendeleo. Pamoja na changamoto zilizopo, serikali inastahili pongezi kwa kazi nzuri inayofanya katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo;

a) Kuonesha uthubutu na dhamira ya dhati katika mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, uvivu, uzembe na kutojali katika sekta zote za serikali
b) Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu kama barabara, reli, usafiri wa anga na mengine.
c) Kuondolewa kwenye mfumo wafanyakazi hewa na wenye vyeti feki ambao walikuwa wanalipwa mishahara na marupurupu mengine isivyo halali.
d) Usimamizi wa nidhamu kwa wafanyakazi wa ngazi zote yaani viongozi wa taasisi na wafanyakazi wa kawaida. Serikali ya awamu ya tano imeondoa viashiria vya miungu watu kwenye taasisi zote za umma.
e) Kipekee kabisa,pongezi kwa Mh. Rais kwa kuingilia kati sintofahamu ya kikokotoo kwa njia shirikishi ya kukaa mezani na viongozi wa vyama vya wafanyakazi kikiwemo THTU ambayo haipo kwenye TUCTA.

5 HITIMISHO

Tunapenda kuhitimisha uchambuzi wetu kwa kuweka bayana kwamba, ili tufanikiwe, tunapaswa kuzingatia yafuatayo:

1) Wafanyakazi tufanye kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, ubunifu na uzalendo ili tufurahie manufaa kwa pamoja
2) Wafanyabiashara wafanye biashara halali kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na serikali. Kila mfanyabiashara aone fahari kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa
3) Wakulima, wafugaji, wavuvi, wajasiriamali na makundi yote yaliyoko katika sekta za uzalishaji waoneshe ubunifu katika shughuli zao ili kuleta tija kwenye bajeti ya taifa na hatimae maendeleo endelevu ya nchi
4) Serikali ijenge mazingira wezeshi ya ufanyaji kazi, biashara, kilimo na shughuli nyingine zote ili hatimae manufaa yaonekane katika maendeleo ya nchi.
5) Serikali itumie wataalamu wa ndani katika masuala mbalimbali ambayo yanawezekana kufanywa na wazalendo.
6) Serikali kupitia Wizara ya mambo ya ndani ya nchi idara ya Uhamiaji ibadili utaratibu wa utoaji wa hati ya kusafiria ya muda mfupi (emergency travel document). Utaratibu wa zamani wa kutoa kibali hicho kwa mwaka mmoja urejeshwe ili kutowafungia Watanzania milango kufanya biashara na nchi nyingine za Afrika mashariki. Ifahamike kwamba, nchi tatu za Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Uganda na Rwanda zimekubaliana kutambua kitambulisho cha Utaifa cha raia wao kama hati ya kusafiria katika nchi hizo.Tusiwabane watanzania katika kuwasiliana na wenzao

Mwisho kabisa;

Serikali ione umuhimu na ulazima wa kulipa malimbikizo na stahiki mbalimbali ya watumishi wa umma na wadau wengine kwa wakati, ili kupunguza manung'uniko na kuongeza morali na ufanisi wa utendaji kazi kwa makundi yote ili kukuza uchumi na maendeleo ya nchi.

6 REJEA

Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2017

International Telecommunications Union (ITU), *Global Cybersecurity Index (GCI)* 2017,

SERIANU (2016) *Cyber Security Report* 2016

The United Republic of Tanzania (2016) National Information and Communications Technology Policy (NACTP 2016)

Chama cha Mapinduzi (2015) *Ilani kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015*

The United Republic of Tanzania (2015), *The Cybercrime Act* 2015.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2018), *Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 116*

World Bank (2019), *Doing Businesss Report 2019.*

Bunge la Tanzania. *(2018). Hotuba Ya Waziri Wa Fedha Na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango (Mb), Akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2019/20.*

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Uwazi-Twaweza (2010),*Taarifa ya misamaha ya kodi Tanzania 2010.*

The United Republic of Tanzania (2012), *Income tax act 2012*

The United Republic of Tanzania (2018), *Finance act 2018/19*

WAJIBU – Institute of Public Accountability, Ripoti Ya Uwajibikaji 2015 - 16